TANGAZO LA SERIKALI NA. 433 la tarehe 17/6/2022

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16 (1)*

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) (MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA, 2022

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) (Marekebisho) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za Mwaka 2022, na zitasomwa pamoja na Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za Mwaka, 2020 ambazo zitajulikana kama Sheria Ndogo Kuu na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Marekebisho GN Na. 777 ya tarehe 18/09/2020

2. Marekebisho yamefanyika katika Sheria Ndogo Kuu kwakufuta kipengele cha 16 cha Jedwali la Kwanza na sehemu ya 16 kipengele cha 9 cha jedwali la kwanza kama inavyoonekana katika.

3. Marekebisho yamefanyika katika Sheria Ndogo kuu kwa kufuta sehemu ya 16 kipengele cha 8 cha Jedwali la kwanza.

4. Marekebisho yanafanyika katika Sheria Ndogo kuu kwa kufuta Sehemu ya 16 kipengele cha 9 cha Jedwali la Kwanza.

5. Marekebisho yanafanyika katika Sheria Ndogo Kuu sehemu ya 13 Kipengele cha 19 katika

Jedwali la Kwanza kwa kuongeza maneno ***"kwenye sherehe na matukio ya kibiashara"*** mara baada ya neno picha.

6. Marekebisho yanafanyika katika Sheria Ndogo kuu sehemu ya 13 Kipengele cha 18 cha Jedwali la Kwanza kwa kuongeza maneno ***"kwenye sherehe na matukio ya kibiashara"*** mara baada ya maneno vyakula.

7. Marekebisho yanafanyika katika Sheria Ndogo Kuu sehemu ya 13 ya jedwali la kipengele cha 1 na 2 kwa kuongeza maneno ***"kwa wasanii wakubwa wenye hadhi ya kitaifa"*** mara baada ya maneno tamasha na kongamano.

Lakiri ya Halmashauri imegongwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa katika mkutano mkuu wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Jiji la Mbeya uliofanyika mnamo tarehe…………Mwezi …………., 2022 na lakiri iliyogongwa na kushuhudiwa na:-

TRIPHONIA KISIGA,
*Kaimu Mkurugenzi,*
*Halmashauri ya Jiji la Mbeya*

DORMOHAMED ISSA RAHMAT,
*Meya*
*Halmashauri ya Jiji la Mbeya*

NAKUBALI,

**L.S**

INNOCENT LUGHA BASHUNGWA (MB)
*Waziri wa Nchi-Or-Tamisemi*